JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

Multisectoral magazine

MACHI 2022 | ISSUE NO 002



Siku

# 365

# NCHI Imefunguka

TSHS. 9,000 KSHS.446 USHS 13,800

5 901234 123457

ISSN 2799-225X | LESENI 00000021

www.tz&beyond.co.tz

# KCB BANK


Internet Banking
I-Bank
Agency Banking
ATM
Mobile Banking
Mobi
TISS
EFT
TT
Government Electronics Payments (GEPG)
E.A Payments
Let's talk
Internet Banking App
My experience with **KCB Bank** is that of modern times...

# BODI
## YA WAHARIRI


**AFISA MTENDAJI MKUU**

Emmanuel J. Kakuyu
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

**MHARIRI MTENDAJI**

Jimmy C. Kiango
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MSANIFU KURASA**

Felix Jimmy
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MWANDISHI**

Hassan Daud
Cell: 0692 695 889

**MWENYEKITI/MLEZI**

Dk. Thomas Kashililah
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com



**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania



**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com

TZ&BEYOND




38 RAIS SAMIA NI NYOTA YA UONGOZI





07 Siku 365 nchi imefunguka



07 Mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Sh Trilioni 1.447,



30 Wanawake kwenye vyombo vya maamuzi



44 Mwaka mmoja wa Rais Samia kama miaka 11



26 Upatikanaji wa dozi ya corona





21
Sekta ya utalii kufunguka



16 Nchi kufunguka kimataifa



34 Uendelezaji urafiki kimataifa



36
Serikali imetenga Bill. 1.5 kwa ajiri ya michezo na sanaa



22
Uendelezaji wa miradi ya kimkakati



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na Mwanamfalme wa Abu Dhabi na Naibu Kamanda wa Majeshi ya Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)


MRADI WA NYUMBA1000 DODOMA
NYUMBA 300 ZINAUZWA
IYUMBU SATELLITE CENTRE II
NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU
Wahi sasa!
Nyumba ni Chache
Nyumba 150 za vyumba viwili zenye ukubwa wa mita za mraba 120
Nyumba 100 za vyumba vitatu zenye ukubwa wa mita za mraba 100
Nyumba 50 za vyumba viwili zenye ukubwa wa mita za mraba 75
+255 736 114 433
www.nhc.co.tz



# Siku 365 NCHI Imefunguka


HOUSE

KIPINDI cha siku 365 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na timu yake kimeifungua nchi katika uchumi wa kitaifa na kimataifa.

Kipindi hicho ambacho ni takribani miezi 12 kikijumuisha Machi 19,2021 hadi Machi 19,2022, kinasafari ndefu.

Rais Samia, alikabidhiwa kiti cha urais, Machi 19,2021, wakati huo nchi ikiwa katika lindi la majonzi na huzuni. Hali ilikuwa hivyo kufuati kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, mwanamapinduzi Hayati Dkt. John Magufuli. Dkt. Magufuli alifariki duniani Machi 17,2021 kwenye hospitali ya Mzena, jijini Dar es Salaam kwa kile kilichodaiwa kuwa ni ugonjwa wa moyo. Kifo hicho kilitoa nafasi ya moja kwa moja kwa Makamu wa Rais ambaye kwa wakati huo alikuwa ni Samia suluhu Hassan kukabidhiwa kiti cha urais kwa mujibu wa kifungu cha 37(5) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotungwa mwaka 1977. Machi 19,2021 safari ya uongozi wa mama Samia ilianza rasmi akiwa kama Rais wa Tanzania. Jambo la kufurahisha mwanzoni tu mwa uongozi wake mara baada ya kufikisha siku 100 jamii ilianza kumtazama kiongozi huyu kwa tabasamu pana la matumaini. Uongozi wake katika siku 100 za awali na baadae mwaka mmoja unatajwa kubeba taswira pana ya matumaini mapya kwa watanzania wengi. Ushirika na muungano wa kiuongozi na kiutendaji wa Rais Samia na viongozi wenzake wakuu wa dola kwa maana ya Bunge na Mahakama umelifanya taifa kuendelea kuwa katika kiwango cha juu cha umoja, mshikamano, amani na tulivu.

Aidha uteuzi wa Dk. Philip Mpango kwenye nafasi ya Makamu wa Rais na Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu uliibua hamasa zaidi kwa wananchi wengi hasa wanaoujua na kuuthamini mchango wa viongozi hao wawili ambao walikuwa vinara wa mafanikio ya serikali ya awamu ya Tano.

Uwepo wa viongozi hao, pamoja na ushirikiano wao wa karibu na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi umedhihirisha kuwapo kwa tumaini jipya la maisha kwa wafanyabiashara wakubwa, wa kati, wadogo, watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla wake Bara na Visiwani.

Na JIMMY KIANGO
@Tz&beyond@gmail.com

DONDOO

## Katika kipindi chake mambo mengi yamefunguka

Mengi aliyoyafanya bila kujali kama ni yale yaliyoachwa au ni mapya yamesaidia kwa sehemu kubwa kuifungua nchi kwenye mambo muhimu na yanayogusa maisha ya kila siku ya mtanzania. Katika kipindi chake hicho amelifungua taifa kwenye eneo la Muungano kwa kuondoa kero zaidi ya 11, kuimarisha uchumi wa nchi na wananchi, kuruhusu Uhuru wa kutoa maoni na kufungua milango ya ushirikiano Kimataifa. Mengine ni kuendeleza miradi yenye maslahi kwa mwananchi, kurejesha imani kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kutafuta ahueni ya riba za mikopo kwa wafanyabiashara, kupunguza kodi na tozo, kuipiga jeki sekta ya utalii na kumwaga maelfu ya ajira kwa vijana na wataalamu mbalimbali pamoja na kupandisha vyeo watumishi wa umma wenye sifa.

**Mengi aliyoyafanya bila kujali kama ni yale yaliyoachwa au ni mapya yamesaidia kwa sehemu kubwa kuifungua nchi**



## "Ameweza kuendeleza vile vilivyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Dkt. Magufuli pamoja na kuanzisha mapya lukuki.

Timu hii ya uongozi imefanikiwa kulivusha taifa katika nyakati ngumu ambazo wakosoaji wengi wa ndani na nje ya nchi walitegemea matokeo hasi.

Ikumbukwe kuwa Serikali ya awamu ya Sita ilichukua uongozi katikati ya mfumo uliojipambanua kuwapigania wanyonge.

Mfumo uliotazamwa kama kimbilio la walala hoi huku ukibebeshwa sura ya kuwa mfumo hatari na usio rafiki kwa matajiri.

Fikira zote hizo zilichangiwa pakubwa na dhana ya mfumo dume ambayo iliwaongoza wakosoaji kujiaminisha kuwa hataweza.

Aidha mazowea ya nchi kuongozwa na wanaume kabla na hata baada ya Uhuru wa Tanganyika, Zanzibar na baadae Tanzania nayo yalichagiuza fikra hizo.

Mtazamo na fikra hizo, ulikoleza kasi ya baadhi ya watu kukosa imani kwa mwanamama huyu hodari.

Pamoja na baadhi ya wakosoaji wake kuutambua vema uwezo wake wa kiuongozi tangu akiwa waziri katika serikali za pande zote mbili Bara na visiwani, Makamu Mwenyekiti Bunge Maalum la Katiba na baadae Makamu wa Rais, bado waliamini hawezi.

Kukosekana kwa imani dhidi yake kulimsukuma yeye mwenyewe kusimama hadharani Machi 22,2021, jijini Dodoma wakati wa kuuaga kitaifa mwili wa Hayati Magufuli na kuieleza hadhira kuwa aliyesimama mbele yao ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"...kwa wale ambao wana mashaka mwanamke huyu ataweza kuongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nataka niwaambie huyu aliyesimama hapa ni rais, wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania ambaye maumbile yake ni mwanamke..,"

Kauli yake hiyo pamoja na maamuzi yake kadhaa ya haraka, yaliwarudisha nyuma wakosoaji na wapingaji wa uongozi wake walioanza kujitokeza ndani na nje ya chama chake CCM na wachache wakiwa serikalini. Pamoja na kuwa na haiba ya upole na sauti ya taratibu isiyofoka wala kung'aka, Rais Samia ameonesha uwezo wa hali ya juu kiutendaji huku akitumia zaidi kalamu katika kuwawajibisha wale wote wasioendana na kasi yake. Hatua hiyo inamuweka kwenye hostoria ya kufanya mambo mengi mazuri katika kipindi cha mwaka mmoja.

Ameweza kuendeleza vile vilivyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Dkt. Magufuli pamoja na kuanzisha mapya lukuki. Mengi aliyoyafanya bila kujali kama ni yale yaliyoachwa au ni mapya yamesaidia kwa sehemu kubwa kuifungua nchi kwenye mambo muhimu na yanayogusa maisha ya kila siku ya mtanzania. Katika kipindi chake hicho amelifungua taifa kwenye eneo la Muungano kwa kuondoa kero zaidi ya 11, kuimarisha uchumi wa nchi na wananchi, kuruhusu Uhuru wa kutoa maoni na kufungua milango ya ushirikiano Kimataifa.



WAZIRI MKUU, KASSIM MAJALIWA AKIZUNGUMZA BAADA YA KUKAGUA UJENZI WA IKULU YA CHAMWINO JIJINI DODOMA

PICHA | OFISI YA WAZIRI MKUU





UJENZI WA IKULU YA CHAMWINO, JIJINI DODOMA
PICHA | OFISI YA WAZIRI MKUU

DONDOO

## Katika kipindi chake hicho amelifungua

Mengine ni kuendeleza miradi yenye maslahi kwa mwananchi, kurejesha imani kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kutafuta ahueni ya riba za mikopo kwa wafanyabiashara, kupunguza kodi na tozo, kuipiga jeki sekta ya utalii na kumwaga maelfu ya ajira kwa vijana na wataalamu mbalimbali pamoja na kupandisha vyeo watumishi wa umma wenye sifa.
Kutokana na uhodari wa serikali ya awamu ya Sita Jarida la TZ&BEYOND limezifanyia rejea na kuzichambua siku 365 za uongozi wa Rais Samia kama ifuatavyo:-





RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN AKIZUNGUMZA NA KUAGANA NA MWENYEJI WAKE RAIS WA UFARANSA MHE. EMMANUEL MACRON. PICHA IKULU






DONDOO

## Katika kipindi chake mambo mengi yamefunguka

Kutokana na uhodari wa serikali ya awamu ya Sita Jarida la TZ&BEYOND limezifanyia rejea na kuzichambua siku 365 za uongozi wa Rais Samia kama ifuatavyo:-

### KUIFUNGUA NCHI KIMATAIFA

Eneo hili limekuwa na mafanikio makubwa kwa nchi, hasa ikizingatiwa kuwa mtangulizi wake hakuwa kiongozi mwenye kupenda kusafiri nje ya nchi.

Hadi kufikia Machi 19,2022, Rais Samia alishafanya ziara za kikazi zaidi ya 10 katika mataifa mbalimbali duniani sanjari na kupokea viongozi mbalimbali wa nchi na mashirika ya kimataifa.

Jarida la TZ&BEYOND linakuorodheshea baadhi ya safari hizo.

### MEI 4, 2021-KENYA

Katika ziara hiyo ya siku mbili, Rais Samia aliitumia kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Mei 5, 2021, akiwa katika mwendelezo wa ziara yake nchini humo, Rais Samia alipata kusema kuwa anakwenda kufungua nchi kwa sababu amekuwa akitukanwa sana kwenye mitandao kuwa anakwenda kubomoa yaliyojengwa kwa muda mrefu.

### APRILI 11,2021- UGANDA





Ziara ya Kenya ilitanguliwa na ile ya Uganda aliyoifanya Aprili 11, 2021, ikiwa ndio ziara yake ya kwanza tangu achukue usukani wa urais.

### JUNI 22, 2021-MSUMBIJI

Rais Samia alikwenda nchini Msumbiji kuhudhuria Mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya SADC.

### JULAI 16,2021-BURUNDI

Moja ya faida nyingi za ziara hiyo ya siku mbili ni ujenzi wa kiwanda cha Mbolea cha Itracom Fertilizer Limited jijini Dodoma.

### AGOSTI 2,2021-RWANDA

Ilikuwa ni ziara ya siku mbili, ambapo Rais Samia, alitembelea kiwanda cha utengenezaji wa simu za kisasa za mkononi.

### AGOSTI 16,2021-MALAWI

Ilikuwa ni ziara ya kikazi kwa Rais Samia kuhudhuria Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Agosti 17-18, mwaka huu.

### AGOSTI 24,2021-ZAMBIA

Ziara hii ya Rais Samia haikuwa ya kikazi, bali ililenga kuhudhuria sherehe ya kuapishwa kwa Rais mpya wa saba wa Zambia, Hakainde Hichilema.

### SEPTEMBA 18,2021-UNGA

Rais Samia alielekea jijini New York kuhudhuria Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA).

### OKTOBA 30,2021- SCOTLAND

Rais Samia alielekea nchini humo kuhudhuria Mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa (UN-COP 26) uliojadili athari za mabadiliko ya tabianchi, pamoja na jitihada za kupunguza kiwango cha uzalishaji wa hewa ya ukaa ili kupunguza joto duniani.

### NOVEMBA 10, 2021-MISRI

Ilikuwa ni ziara ya siku tatu iliyotokana na mwaliko wa Rais wa Misri, Abdel Fattah Al Sisi. Ililenga kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa hayo katika nyanja mbalimbali, ikiwamo diplomasia, uchumi, ulinzi, siasa, na utalii.

### FEBRUARI-UFARANSA,DUBAI

Aidha baadhi ya ziara nyingine muhimu zilifanyika Februari 2022, nchini ufaransa na Dubai, ambazo zimeshaanza kuleta tija kutokana na kuibuka kwa wimbi kubwa la wawekezaji kutoka kwneye nchi hizo.

### MAMBO YA MUUNGANO

Kwa miaka mingi, licha ya pande zote mbili, kwa maana ya Bara na Visiwani, kuweka nguvu kubwa katika kulinda na kudumisha Muungano, Rais Samia amepiga hatua moja mbele kwa kutumia muda mfupi kutatua changamoto 11 zilizokuwa kero.

### UCHUMI SHIRIKISHI

Katika kipindi hiki cha utawala wa Rais Samia, licha ya tishio la janga la Uviko-19, siku 365 za serikali yake zimeshuhudia hatua mbambali za kuimarisha uchumi zikichukuliwa.

### PATO LA TAIFA

Kumekuwa na ukuaji wa Pato la Taifa na mfano wake ni kwenye Robo ya Pili ya Mwaka 2021, ambapo kutoka Aprili mpaka Juni, 2021, uchumi uliongeza na kufikia asilimia 4.3, ukilinganisha na asilimia 4 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Udhibiti wa mfumuko wa bei uliendelea kuwa na tarakimu moja. Aidha, katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Septemba, 2021, mfumuko wa bei ulikuwa kwa wastani wa asilimia 4.

Kufikia Agosti, 2021, akiba ya fedha za kigeni ilipanda na kufikia Dola za Marekani bilioni 5.8. tofauti na mwaka 2020, ambapo ilikuwa Dola za Marekani bilioni 4. 9.

Ukusanyaji wa mapato umekuwa ukiongezeka mwezi hadi mwezi, ambapo kuanzia Mwezi Aprili hadi Septemba, 2021, Serikali ilikusanya Sh Trilioni 9.905.

Mapato yasiyokuwa ya kodi yalikuwa Sh Trilioni 1.436, hivyo kufanya jumla ifikie Sh Trilioni 11.41, sambamba na mikopo ya masharti nafuu, ukiwamo wa Sh Trilioni 1.447. Serikali iliweza kutoa kiasi cha zaidi ya Sh. Trilioni 8.243 kutekeleza miradi na shughuli za maendeleo. Aidha imeweza kulipa madeni ya nje na ya ndani. Uhakiki wa madeni ya ndani (Tsh bilioni 439) yanayotokana na watumishi, wazabuni wakubwa na wadogo, wakandarasi wakubwa, huduma za umeme, maji na simu kwa taasisi za umma, na fidia na malipo ya bima za ajali.

**"Ameweza kuendeleza vile vilivyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Dkt. Magufuli pamoja na kuanzisha mapya lukuki.**

### UWEKEZAJI

Serikali iliondoa urasimu kwenye utoaji wa vibali vya kazi kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki au E-Permit, ambao kwa kiasi kikubwa umepunguza siku za utoaji vibali. Vilevile, imekamilisha mchakato wa kuunda dirisha moja la kielektroniki la uwekezaji, yaani Electronic Single Window For Investment, kituo cha mawasiliano kuhusu masuala ya uwekezaji na pia kanzi data ya ardhi yenye ukubwa wa hekta 1.6 milioni.

Kumekuwa na uimarishwaji wa majadiliano na sekta binafsi, ambapo serikali ilifanya mkutano na Baraza la Taifa la Biashara.

Kutokana na hatua hizo, miradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 3.5, ambayo inatarajia kuzalisha ajira 43,782 imesajiliwa na hivyo kusaidia kupunguza tatizo la ajira nchini.

Aidha miradi 164 yenye thamani ya Dola za Kimarakeni bilioni 3.158 imesajiliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC) na miradi 18 imesajiliwa na EPZA.

Kwenye kipindi kama hicho mwaka uliopita, ilisajiliwa miradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 647.43.

Kwa upande wa biashara, mauzo ya bidhaa za nje katika kipindi cha Machi hadi Agosti, 2021, yaliongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 3.4 kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.4 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Aidha, BRELA ilitoa leseni za biashara 6,051, hii inamaanisha kumekuwa na ongezeko la biashara ndani ya nchi.

Nchi pia imeridhia mkataba wa kujiunga na Eneo Huru la Biashara Afrika, ambalo litaongeza soko kwa wafanyabiashara wa ndani.

### MIRADI

Ipo miradi mingi ambayo inaendelezwa na mingine kuanzishwa na serikali ya awamu ya sita, baadhi yake ikiwa ni:-

### KILIMO NA UVUVI

Siku 365 zimeshuhudia uhakiki wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 237941.9 na kupima afya ya rutuba ya udongo, ujenzi wa vihenge vya kuhifadhia mazao, ukarabati na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, uanzishaji wa masoko na kufungua vituo vya kuuza mazao nje ya nchi (Kenya, Sudan ya Kusini, China, India, Ukraine, Umoja wa Ulaya, nchi za SADC na Saudi Arabia) na kulifanya Ghala la Taifa la Chakula (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko zipate Sh bilioni 129.

Serikali pia ilitoa Sh bilioni 100 kwa NFRA na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ili kununua mahindi kwa wakulima kwa bei nzuri (kutoka Sh 300 hadi Sh 500 kwa kilo). Mafanikio ya Serikali yalikuwa ni kukamilisha Kituo cha Ukuzaji viumbe-bahari, samaki mwani, majongoo ya bahari na



#### MIFUGO
Chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, viwanda vipya sita vya kusindika maziwa vimekamilika, kikiwemo cha Dodoma Halisi.

#### VIWANDA
EPZA ilitoa leseni kwa kampuni 18 na pia viwanda vidogo 374 vimeanzishwa. Aidha, mradi wa Industrial Trande and Logistic Center Kurasini, jijini Dar es Salaam nao pia umeanza.

#### UTALII
Sekta hii imekumbana na dhoruba la UVIKO-19 lakini Serikali ya Awamu ya Sita imepambana vya kutosha kuipa uhai.

Angalau sasa idadi ya watalii wanaokuja nchini imeanza kuongezeka, ambapo kuanzia Machi hadi Septemba, 2021, jumla ya watalii 46,913 wametembelea Tanzania.

Katika kuipambania zaidi sekta ya utalii, Rais Samia ameingia kwa miguu miwili kwenye kipindi maarufu duniani cha 'Royal Tour', ambapo ataonekana yeye mwenyewe akiwatembeza watalii kwenye vivutio mbalimbali vya utalii Tanzania.

Juhudi kubwa za kimkakati za Royal Tour zilizoendeshwa na Rais zimeweza kuzaa matunda, ambapo kumekuwa na ujio wa wawekezaji kutoka Bara la Ulaya ambao wamejenga hoteli tatu za nyota tano za 'brand' ya Kempiski kwa uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 72.






# Utalii

(TZ&BEYOND LITATOA JARIDA MAHSUSI JUU YA ROYAL TOUR)

**Katika kipindi cha mwaka mmoja, serikali imeendeleza ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam - Morogoro, ambao umefikia asilimia 93 na Morogoro – Makotopora ambao umefikia asilimia**

**70**

### USAFIRISHAJI

Katika kipindi cha mwaka mmoja, serikali imeendeleza ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam - Morogoro, ambao umefikia asilimia 93 na Morogoro – Makotopora ambao umefikia asilimia 70.

Hiyo ni nje ya kuanza ujenzi wa kipande cha Mwanza-Isaka, ambao kwa pamoja kiasi cha Sh Trilioni 1.32 kimetumika. Usafiri wa barabara nao haukusahaulika ndani ya siku 365, barabara nyingi zinaendelea kujengwa, ikiwamo ya mzunguko ya njia nne jijini Dodoma, kama ambavyo itafanyika Singida; upande wa kwenda Iringa, upande wa kwenda Dar es Salaam, na upande wa kwenda Arusha. Kupitia TARURA, Serikali ilitumia Sh bilioni 219 na milioni 39 kufanya matengenezo ya barabara vijijini, ambazo nyingi ziliharibiwa na mvua msimu uliopita. Serikali imetoa Sh bil 1.5 kwenye kila jimbo kwa ajili ya uwekaji wa lami, hasa kwenye barabara za miji.

### USAFIRI WA MAJI

Septemba, 2021, serikali ilikamilisha ujenzi wa gati namba moja hadi saba kwenye Bandari ya Dar es Salaam na kazi ya kupanua, kuchimba na kuongeza kina inaendelea. Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala -Ruvu umefikia zaidi ya asilimia 58 na ujenzi wa meli mpya kwenye Ziwa Victoria umefikia zaidi ya asilimia 80.1.

Kwa upande mwingine, Juni, 2021, Serikali ilisaini mikataba mitano kwa ajili ya ukarabati wa meli ya mizigo ya MV Umoja, ujenzi wa meli nyingine mpya ya kubebea mabehewa ya mizigo kwenye Ziwa Victoria na pia meli mpya ya abiria na mizigo katika Bahari ya Hindi na meli ya mizigo, pamoja na ukarabati wa meli ya kubeba mafuta ya MT Sangara Ziwa Tanganyika, mkataba huo umejumuisha meli tano.

Miradi hii yote ya ujenzi na ukarabati wa meli ina thamani ya Sh bilioni 317.484.



### USAFIRI WA ANGA

Septemba 2021, Serikali ilisaini mkataba wa kuanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato jijini Dodoma, huku upanuzi wa viwanja vingine, kikiwamo cha Mtwara, Songea na Iringa, ukiendelea.

Ni hatua iliyokwenda sambamba na ununuzi wa ndege tatu, hivyo kufikisha idadi ya ndege 11. Pia, Serikali imesaini mkataba wa ununuzi wa ndege nyingine tano, ambazo zitagharimu Sh bilioni 596.3.















NISHATI NA MADINI

Ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere umefikia asilimia 55.6, ambapo Sh bilioni 696.76 zimetumika kati ya Mwezi Aprili hadi Septemba, 2021.

Pia, zimetumika Sh bilioni 112.9 kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka bwawa hilo kwenda Chalinze kwenye kituo kikubwa.

Kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Singida-Arusha-Namanga umefikia asilimia 96.1. Ndani ya kipindi hicho, vijiji 312 vimefikishiwa huduma ya umeme, huku 1974 vilivyosalia vikitarajiwa kufikishiwa ifikapo Desemba, mwakani.

Katika kipindi cha Aprili hadi Septemba, 2021, pia Rais Samia na utawala wake wameweza kukamilisha mikataba yote muhimu ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda, hadi Tanga na Serikali imetoa Sh bilioni 259.96 kununua hisa kwa asilimia 15 za umiliki wa Bomba hilo. Katika kipindi cha Machi hadi Septemba, 2021, jumla ya leseni 5,126 zimetolewa,




ikilinganishwa na leseni 3,195 kipindi kama hiki mwaka 2020. Kati ya leseni hizo, tatu ni za uchimbaji mkubwa, nazo ni zile leseni za Nyanzaga- Sengerema, Pick Resources Songwe, na Tembo Nickel.

Kama hiyo haitoshi, leseni 1001 ni za uchimbaji mdogo.

Serikali imekusanya Sh bilioni 336.5 katika madini, pia ikikamilisha ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kusafisha dhahabu jijini Mwanza, ambacho kitatumia kilo 480 kwa siku.

### TEKNOLOJIA YA HABARI

Serikali imefanikisha ujenzi wa kilometa 409 za Mkongo wa Taifa, kufikisha mawasiliano katika kata 132 na kuongeza idadi ya kata zilizowekewa miundombinu ya anuani ya makazi kutoka 117 hadi kufikia 135.

Serikali pia imeondosha VAT kwenye simu-janja, vishikwambi, na moderm, hivyo kuongeza watumiaji wa simu kutoka milioni 52.9 hadi milioni 55.4.

## AFYA

Serikali ilifanikisha upatikanaji wa dozi za Corona 1,518,400 kutoka kwa Serikali ya Marekani na dozi 1,065,000 kutoka Covax Facility.

Kufikia Oktoba 5, 2021, wananchi waliochanja walifikia 846,000. Serikali pia imejenga kiwanda cha kutengeneza vifaa vya kujikinga na maradhi hayo jijini Dar es Salaam.

Vilevile, sekta ya afya imenunua dawa zenye thamani ya Sh bilioni 234, na vifaa-tiba vya Sh bilioni 26.3, mashine ya kupasulia ubongo bila kufungua kichwa katika Taasisi ya MOI, Sh bilioni 7.9 , kuendeleza ujezi wa miradi 25 ya hospitali za Rufaa, Mikoa na Kanda.

Tozo ya miamala ya simu nazo ziliisaidia Serikali kutoa Sh bilioni 37.5 kujenga vituo vya afya katika tarafa 150 kati ya tarafa 207, ambazo hazina vituo vya afya.

## ELIMU

Serikali ilichangia Sh bilioni 145. 58 kugharamia elimu bila malipo. Sh bilioni 208.49 zilitumika kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu.

"Kuhusu mikopo hiyo, kwenye Bajeti ya Mwaka huu wa Fedha, tumeongeza kiwango ili kila anayestahiki kupata huduma hiyo aweze kunufaika na huduma hiyo," alisema Rais Samia.

Mei, 2021, Serikali ilipata mkopo wa Sh bilioni 972 kutoka Benki ya Dunia ili kuimarisha elimu kwenye vyuo vikuu 14.

Pia, kuna ujenzi wa chuo kikubwa cha ufundi jijini Dodoma kwa gharama ya Sh bilioni 18, na Sh bilioni 40 za kujenga vyuo vya ufundi stadi kwenye wilaya 25.

Serikali imetumia Sh bilioni 120 kujenga miundombinu ya shule za msingi na sekondari, ambapo Sh bilioni 7 zimetokana na Tozo za miamala ya simu ambazo zimejenga madarasa 560 ya shule za sekondari.

Serikali ilibainisha kuwa kwa mwaka 2021, wanafunzi waliomaliza darasa la saba ni takribani 1000,000 na wanaomaliza kidato cha nne ni 400,000, hivyo kuna ongezeko la wanafunzi 500,000.











sekta ya afya imenunua dawa zenye thamani ya Sh bilioni 234, na vifaa-tiba vya Sh bilioni 26.3, mashine ya kupasulia ubongo bila kufungua kichwa katika Taasisi ya MOI, Sh bilioni 7.9



Mafanikio Mengine ya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye sekta ya elimu ni kujenga shule 10 za masomo ya Sayansi kwa wasichana zenye thamani ya Sh. bilioni 20 kwenye mikoa 10. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Kagera, Lindi, Pwani, Tanga, Songwe, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Mwanza. Shule hizo 10 kila moja itagharimu kiasi cha sh. milioni 600 .

Aidha serikali kupitia Tamisemi ilitoa Bilioni 109.7 kujenga shule 234 za Kata, ambapo kila kata moja kwenye majimbo 214 itapata shule na nyingine 20 kwenye halmashauri zenye uwiano mkubwa wa wanafunzi darasani huku kila moja ikigharimu Sh. milioni 600 .

### MAJI

Serikali imetumia Sh bilioni 352 kutekeleza miradi ya maji. Katika kipindi hicho, jumla ya miradi 328 (miradi 311 vijijini na 17 mijini ) yenye thamani ya Sh bilioni 109.125 imekamilika na kunufaisha wananchi wapatao 2,300,000 (wananchi 1,975,197 vijijini na 372,002 mijini).

### HAKI

Jumla ya mashahuri 104,141 yalisikilizwa katika ngazi mbalimbali za mahakama. Katika kupunguza mrundikano wa kesi, Rais Samia aliteua majaji wapya wa Rufaa saba na Mahakama Kuu 21, na pia kuwaajiri mahakimu 245. Hii iliongeza idadi ya majaji wa rufaa kutoka 17 hadi 24 na wa mahakama kuu kutoka 69 hadi 84. Hilo liliambatana na ukamilishaji wa vituo jumuishi vya utoaji haki sita vilivyogharimu Sh bilioni 51.53, Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi na Mahakama za Wilaya ya Bunda, Chemba na Bahi.

Ukarabati wa Mahakama Kuu moja na za Hakimu Mkazi mbili na za wilaya tisa unaendelea, huku Ofisi ya Taifa ya Mashitaka ikifungua ofisi za wilaya tatu pale Kilombero, Serengeti na Karagwe. Ofisi ya Taifa ya Mashitaka iliondoa mashahuri 467 kwa kukosekana ushahidi wa kutosha, achilia mbali Serikali kutumia njia mbadala za maridhiano, upatanishi na usuluhishi. Tanzania ilishiriki vikao vya Kikanda barani Afrika na ulimwenguni. Pia, TAKUKURU kupitia operesheni zake ilifanikiwa kuokoa kiasi cha Sh bilioni 2.750 na kukamilisha uchunguzi wa majalada 312 na kufungua kesi 240 mahakamani.

**Serikali imetumia Sh bilioni 352 kutekeleza miradi ya maji.**


TIB
DEVELOPMENT
BANK
Your Partner for Growth
Chagua Benki ya Maendeleo TIB
Mshirika Wako Katika Maendeleo
Benki inatoa mikopo kwenye:
• Uendelezaji wa miundombinu
• Maendeleo ya Viwanda
• Uchimbaji wa madini
• Mafuta na Gesi
• Huduma
md@tib.co.tz
www.tib.co.tz

# Wanawake
## kwenye vyombo vya maamuzi









### USAWA

Kumekuwa na ongezeko la nafasi za wanawake kwenye vyombo vya maamuzi kwenye taasisi za umma na binafsi.

Sambamba na hayo, nchi imepata heshima kimataifa kwa kuwa kinara wa masuala ya haki za usawa wa kijinsia na kiuchumi.

### MOTISHA

Watumishi 29,900 wameajiriwa, watumishi 180,830 wamepandishwa vyeo na kulipwa stahiki zao, watumishi 8,202 wamebadilishiwa kada, watumishi 30,228 wamelipwa malimbikizo yao ya madeni yenye thamani ya Sh bilioni 55.75. Serikali imepunguza makato ya kodi ya mshahara (PAYE) kutoka asilimia tisa hadi asilimia nane. Mbali ya hilo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, PSSF na NSSF, imelipa mafao yenye thamani ya Sh Trilioni 1.540 na Pensheni ya bilioni 46.93 kwa wanachama wao.

### UMASIKINI

Serikali imeendelea na jitihada za kupambana na umasikini, ambapo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kaya masikini 879, 670 zilipatiwa kiasi cha Sh bilioni 71. 395.

Oktoba, 2021, Serikali ilitangaza kuongeza Sh bilioni 20 kwenye TASAF.

### ARDHI

Hatimiliki 41,533 zimesajiliwa, ikilinganishwa na hatimiliki 34,588 mwaka uliopita. Migogoro ya ardhi 745 ilitatuliwa kwa njia za kiutawala na mashauri 13,991 katika mabaraza ya ardhi.Aidha jumla ya viwanja 232 ,596 na mashamba 353 yamepimwa. Mashamba 11 yenye hekari 24,159 yamebadilishwa na kupangwa kwa ajili ya matumizi mengine, ikiwemo uwekezaji. Serikali imeliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa kupata mkopo wa Sh bilioni 20 ili kujenga nyumba 1,000 jijini Dodoma na pia mkopo wa Sh bilioni 173.9 ili kukamilisha miradi minne ya Morocco Square, Kawe, pamoja na Regency Estates.

**Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha mapitio ya Sera ya Mazingira**

### MAZINGIRA

Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha mapitio ya Sera ya Mazingira na kuandaa Mpango-kazi wa Taifa wa hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa mwaka 2021- 2026.

# Mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Sh Trilioni 1.447, imepatikana



Kuifanyia marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, kuandaa kanuni za udhibiti wa taka hatarishi, kuandaa kanuni za udhibiti wa taka za kielektroniki, kuandaa mkakati wa Taifa wa mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, mashirika yanayoshughulika na mabadiliko ya tabianchi yameshatenga fedha kwa ajili ya Tanzania.

## UFADHILI

Mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Sh Trilioni 1.447, imepatikana huku kukisainiwa mikataba 31 na washirika wa maendeleo yenye thamani ya Sh Trilioni 6.3.

China imetoa ufadhili katika miradi ya umeme na kukamilisha mikataba mikubwa ya ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda, mpaka Tanga.

## VIKWAZO

Kwa muda mrefu kulikuwa na vikwazo visivyo vya kiforodha kati ya Tanzania na Kenya vipatavyo 64.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa utawala wa Rais Samia kwa kushirikiana na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyata wameweza kuondoa vikwazo 46.

Serikali ya Rais Samia imewezesha kupatikana masoko ya bidhaa za nyama ya mbuzi, kondoo na ng'ombe nchini Saudi Arabia na Visiwa vya Comorro, mbogamboga na matunda aina ya Parachichi nchini Qatar.

Lakini pia ameiwezesha Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 65 wa Kamisheni ya Afrika ya Jukwaa la Pili la Uwekezaji.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# ENROLL
# TWIGA MILES
## AND GET 1,000 AWARD POINTS




www.airtanzania.co.tz
airtanzania_atcl








## URAFIKI

Katika kipindi kifupi cha utawala wa Rais Samia, Tanzania imechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, mjumbe wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa, mwenyeji wa Kituo cha SADC cha Uratibu wa Kupambana na Ugaidi.

Katika kuimarisha uhusiano na mataifa mengine, kwa kipindi hiki cha miezi sita, Tanzania imechangia askari 290 na kiasi cha Dola za Marekani 882,873 kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wake kwenye operesheni za ulinzi wa amani katika Jimbo la Cabo Delgado nchini Msumbiji.

Tanzania imefungua ubalozi mpya Vienna, Austria, na Konseli kuu tatu katika miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Shanghai na Guangzhou, China.

Aidha, mabalozi kutoka Czech, Chile, Belarus, Colombia, Ireland, Uturuki, Italia, India, Australia, Ufaransa, Msumbiji, Burkina Faso, Somalia, Nigeria, na Guinea wamewasilisha hati za utambulisho.

Sambamba na hayo, jumla ya mabalozi 23 wameteuliwa na watumishi 137 wamepelekwa katika balozi za nje.

**Mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Sh Trilioni 1.447, imepatikana**


REPUBLIC
NZANIA

# Michezo

## serikali imetenga Bill. 1.5








MICHEZO

Serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo na kutenga Sh bilioni 1.5 kwa ajili ya kusaidia timu za taifa, COSOTA imetengezwa Bajeti ili kuiwezesha kukusanya makusanyo ya wasanii.

Kufutwa kwa VAT kwenye nyasi bandia, kuanzishwa kwa Tamasha la Michezo kwa wanawake, Tuzo za wasanii na kuandaa Tamasha la Afrika la urembo, utanashati na mitindo kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, ni sehemu ya juhudi zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi kifupi ilichokaa madarakani.

"Tumeona ushiriki wa Watanzania katika michezo mbalimbali pamoja na vikundi vilivyoundwa na wanamichezo. Tumeanza kuona mafanikio ya michezo, hasa katika mpira wa miguu na wanamichezo wanaoshiriki michezo hiyo wanaliletea Taifa sifa kubwa kwa timu za wanaume na wanawake," alisema Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa.



Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA **MWANACHAMA NA MWAJIRI**

Mifumo hii ni ya mwajiri **"Employer Portal"** na mwanachama **"Member Portal"** inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko **"www.nssf.or.tz"** bofya kifute cha **"Self Service"** (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa **"Employer Portal"** ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa **"Member Portal"** unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania



# RAIS SAMIA NI *Nyota ya* uongozi



MACHI 19,2022 IMEKAMILISHA SIKU 365 ZA UONGOZI WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, SAMIA SULUHU HASSAN, TANGU AKABIDHIWE KITI CHA URAIS MACHI 19,2021

**Kipindi hiki cha mwaka mmoja cha uongozi wa Rais Samia kinachojumuisha miezi 12, kimeibua nyota njema ya mafanikio kwa nchi na wananchi. Katika kipindi hicho chote mengi yamezungumzwa na kuandikwa,**

MACHI 19,2022 imekamilisha siku 365 za uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, tangu akabidhiwe kiti cha urais Machi 19,2021 kufuatia kifo cha mtangulizi wake Hayati Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kilichotokea Machi 17,2021.

Kipindi hiki cha mwaka mmoja cha uongozi wa Rais Samia kinachojumuisha miezi 12, kimeibua nyota njema ya mafanikio kwa nchi na wananchi.

Katika kipindi hicho chote mengi yamezungumzwa na kuandikwa, wapo waliokuwa na dhana ovu kuwa Rais Samia hataweza kwa sababu ya mazowea yao pamoja na kusukumwa kwao na mfumo dume, mfumo usioamini katika nafasi na fursa ya mwanamke katika ujenzi wa Taifa.

Lakini pia wapo waliodaiwa kujipanga kumkwamisha kwa sababu zao za kisiasa, kibiashara na zaidi kutafuta namna ya kufanikisha maslahi binafsi.

Aidha wapo walioamini nchi imempata mrithi sahihi wa Hayati Dkt Magufuli na huenda kundi hili la mwisho ndilo lililobeba usahihi wa kifikra, kwani Rais huyu ambaye ni wa Sita tangu nchi ipate uhuru Desemba 9,1961, amefanikiwa kuifungua nchi kitaifa na kimataifa pamoja na kufanikiwa kuwaunganisha wananchi wa kada mbalimbali.

Jarida la TZ&BEYOND pamoja na kumpa hongera Rais Samia kwa kufanikiwa, kumudu na kuliongoza vema jahazi la Tanzania, pia tutaziangalia kwa jicho pana siku hizi 365 ambazo kwa kiwango cha juu mbali ya kufungua nchi lakini pia zilibeba ukombozi kwa mtanzania, ambaye sasa hatambulishwi kwa sifa ya unyonge.

Hakuna ubishi wowote Rais Samia Suluhu Hassan ameandika historia ya kutukuka katika Taifa letu, Bara la



**ZIARA YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN GLASGOW NCHINI SCOTLAND** PICHA IKULU

Afrika na duniani kote kwa kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya urais wa Tanzania. Hatua ya Rais Samia kutoka kuwa Makamu wa Rais hadi Rais, inatazamwa kama ni baraka za mwenyezi Mungu kwani haikuwahi kutokea huko nyuma na hakuna aliyefikiria nchi ingepata changamoto ya namna ile ya kuondokewa na ndugu yetu Dk. John Joseph Pombe Magufuli katika kipindi ambacho bado nchi ilikuwa ikimuhitaji. Lilikuwa ni tukio jipya kwa nchi na wananchi kwa ujumla, Tanzania haikuwahi kumpoteza Rais akiwa madarakani. Tukio lile liliwafanya baadhi ya watu waamini kuwa kutakuwa na ugumu katika kumsaka mrithi sahihi wa Hayati Magufuli mwenye uwezo wa kuliziba pengo lake.

Dhana hiyo ilisukumwa na mwenendo na mfumo wa kiutandaji wa Hayati Magufuli. Wengi wa waliowaza hivyo walisahau kama Rais Samia alikuwa ndie msaidizi wa moja kwa moja wa Hayati Magufuli, hatua ambayo inaweza kuelezwa kama alishamuandaa kiongozi wa aina yake kwa miaka zaidi ya mitano. Rais Samia ndiye alistahili na mara ya kwanza katika historia ya nchi, Katiba ilituongoza kufanya uamuzi sahihi na Machi 19,2021 historia mpya iliandikwa.

Kwa sasa tunapofanya rejea ya uwepo wa Serikali ya Awamu ya Sita, kamwe hatuwezi kuziacha nyuma sifa za Hayati Magufuli ambae alileta mabadiliko makubwa ya kiuongozi na kiutendaji nje na ndani ya serikali. Pamoja na kuziangalia siku 365, ikumbukwe kuwa ndani ya siku hizo kulikuwa mambo mengi yaliyogawanyika katika siku na miezi tofauti tofauti.

# TZ&BEYOND

**jarida** hili linalowafikia watu wa rika na kada mbalimbali ndani na nje ya tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.




***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

## *TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO*

**USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI**

www.tz&beyond.co.tz



Ndani ya siku 365 kulikuwa na siku 21 za majonzi na siku 344 za heka heka ambazo ndizo zilizotoa mwelekea wa Taifa kwa mwaka mmoja uliofikiwa Machi 19, 2022 na miaka mitano ijayo.

Pamoja na siku hizo kuwa ngumu, lakini ukweli ni kwamba Rais Samia na timu yake waliweza kuendeleza mshikamano, umoja, uzalendo, amani na utulivu.

Lakini pia kazi iliendelezwa na inaendelezwa kutoka pale ilipoishia kwenye utawala wa Awamu ya Tano.

Kimsingi haikuwa safari rahisi, ilikuwa ngumu iliyohitaji Jemedari mahiri kuongoza jeshi la wachapakazi wenye moyo wa uzalendo, maono, upendo na uvumilivu wa kuweza kumudu kusafiri salama kwa muda wote wa kipindi cha mpito.

Kwa sababu hiyo, Jarida la TZ&BEYOND, tukiwa sehemu ya jamii ya watanzania tuliosafiri pamoja na Rais Samia katika siku 365 za uongozi wake na kufanikiwa kuvuka salama mwaka 2021 tukiwa pamoja na watanzania wengine nyuma yake; tunapenda kutumia fursa hii kumpongeza yeye na watanzania wote.

Jarida la TZ&BEYOND, tukiwa na wajibu ule ule ambao vyombo vingine vya habari vinao wa kuhabarisha jamii, lakini kipekee tukiwa na mtizamo wa kuitakia mema nchi, tunafanya rejea ya utawala wa Rais Samia katika safari hii ngumu lakini yenye mafanikio lukuki.

Historia ni mwalimu mzuri na hiyo ndio itakayomnenea mambo mengi mazuri Rais Samia kuhusu siku 365 za uongozi wake.

Hata hivyo ili historia iandikwe vizuri na kwa usahihi ni lazima ianzie kwenye chimbuko kama ilivyokwishafanyika wakati kutimiza siku 100 za uongozi wake.

Jarida la TZ&BEYOND, tukiwa chombo cha habari makini na chenye dhima adhimu kwa Taifa la Tanzania tunaifanya kazi hiyo ya kuziangazia siku 365.

**Siku**
# 365
**kwa kiongozi mpya kukaa madarakani na kufanikiwa kuliongoza taifa lenye watu milioni zaidi ya 50 si jambo dogo.**

Siku 365 kwa kiongozi mpya kukaa madarakani na kufanikiwa kuliongoza taifa lenye watu milioni zaidi ya 50 si jambo dogo.

Ni jambo lililo wazi kuwa Rais Samia ambaye ameweza kubuni salamu maalum ya nchi ya 'Salaam kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kipokeo chake cha KAZI IENDELEE' ameweza kuulezea umma na dunia kwa ujumla yeye ni kiongozi wa aina gani akitokea kwenye HAPA KAZI TU ya mtangulizi wake.

Falsafa hiyo imejijenga kwenye dhana ya mafanikio aliyopata ndani ya kipindi kifupi cha uongozi wake na kuwapa matumaini watanzania, wawekezaji wa nje na ndani na sekta binafsi kwa kufanyia kazi changamoto walizokuwa wakikabiliana nazo pamoja na urasimu ndani ya Serikali.

Ndani ya jarida hili, pamoja na mambo mengine tutamulika zaidi hatua kubwa za mafanikio zilizopigwa katika kipindi cha siku 365.

Sambamba na hayo, katika chambuzi mbalimbali TZ&BEYOND itaungana na wachambuzi wengine kufanya marejeo ya baadhi ya maagizo na maamuzi magumu aliyoyafanya Rais Samia ndani ya mwaka mmoja.

Kwa mambo ambayo yalitazamwa na wengi jarida hili litayaangazia sanjari na mwenendo wa Dira na Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita, utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyoahidiwa na Serikali yake, halikadhalika mpango wa maendeleo wa miaka mitano na bajeti ya mwaka 2021/2022 inayokwenda kufikia kikomo Julai 1, 2022.

Kwa sasa Tanzania inatajwa kuwa mahali salama, shwari na muafaka kwa kuwekeza kwenye sekta nyingi za kiuchumi na biashara.

Mwekezaji wa ndani na nje ya nchi anaweza kuwekeza kwenye Viwanda, Biashara, Uvuvi, Kilimo, Utalii na Madini.

# MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA KAMA MIAKA 11

Na HASSAN DAUDI
@Tz&beyond@gmail.com

NI Mwaka mmoja sasa tangu Samia Suluhu Hassan aapishwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo katika historia ya Taifa hili, amefanya mabadiliko na mageuzi mengi.

Wasomi na wajasiriamali wawanauzungumzia utendaji kazi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia?

Miongoni mwa wasomi waliomzungumzia ni Dkt. Gasper Mpehongwa, mbobezi wa taaluma ya Mawasiliano ya Umma (Mass Communication).

### DKT. MPEHONGWA

**TZ&BEYOND**: Serikali ya Awamu ya Sita ina muda mfupi madarakani, je, imefanikiwa na tunaweza kuitathmini kwa lipi hasa?

**DKT. GASPER:** Binafsi naiona Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha katika usimamizi wa demokrasia, hasa dhana ya uhuru wa kujieleza.

Wakati wa utawala wa Awamu ya Tano, moja kati ya zilizokuwa zikianishwa kama kasoro ni suala la demokrasia, kwamba ilionekana kama vilikuwapo viashiria vya sauti ya Serikali kuwa yenye nguvu zaidi, huku wakosoaji wakinyimwa fursa ya kutoa maoni yao.

Chini ya Rais Samia, malalamiko ya aina hiyo yamepotea, husikii tena kelele za wanaodai kuminywa. Mfano mzuri ni maagizo yake ya kutaka baadhi ya vyombo vya Habari vilivyofungiwa kutazamwa upya na ikiwezekana vifunguliwe ili viendelee na majukumu yake.

**TZ&BEYOND:** Dkt. Hudhani kama lipo kundi la watu ambalo hutumia uhuru wa kutoa maoni vibaya kwa kuitukana serikali, kama ambavyo sasa wapo wanaomsema vibaya Rais kwa makosa ya awamu zilizopita?

**DKT. GASPER:** Ni kweli, wapo watu wanaoutumia uhuru huo vibaya, lakini nitoe angalizo, hakuna sababu hata moja ya kuutumia uhuru wa kujieleza uliopo kwa miezi nane ya utawala wa Rais Samia kutulewesha hadi kufikia hatua ya kuutumia vibaya.

Waingereza wana msemo wao, 'too much is harmful'. Kwamba kila kitu hakitakiwi kuzidi ili kutoleta madhara badala ya faida. Uhuru huu usiwe wa kupitiliza, ikafika kipindi mtu akajiona ana haki ya kuingilia uhuru wa mwingine.

Mwisho wa uhuru wako ni pale unapoanza uhuru wa mwenzako. Hii ina maana gani? Kwamba uhuru wa kujieleza haukupi haki ya kukashifu na kushusha hadhi ya mwingine au mamlaka zilizoko.

### DKT. JOSEPH MATIKO (DIT)

TZ& BEYOND pia lilifanya mahojiano na Dkt. Joseph Matiko, Mhadhiriwa Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa RAFIC (Regional Flagship ICT Center), unaoendelea chuoni hapo ukiwa na dhima ya kuimarisha umahiri wa TEHAMA nchini.

**TZ&BEYOND:** Hali ikoje kwenye eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kipindi cha miezi nane ya Serikali ya Awamu ya Sita?

## WANANCHI WAWANAUZUNGUMZIA UTENDAJI WAKE



**DKT. MATIKO:** Mengi yamefanyika yanayotoa taswira nzuri ya kasi ya sekta hiyo. Kwanza tukubaliane kuwa TEHAMA imekuwa ikigusa kila hatua ya maendeleo ya jamii, Taifa na dunia kwa ujumla.

Si Tanzania tu, duniani kote, sasa hivi hakuna namna ya kutenganisha maendeleo na utumizi wa simu, kompyuta na vifaa vingine. Sasa nije kwenye miezi nane ya Rais Samia. Kwa utafiti wa kawaida tu, vijiji ambavyo vimepatiwa umeme kipindi hiki, moja kwa moja vimejikuta vikiwa na ongezeko la watu wanaotumia simu, kompyuta n.k. Kwa kweli niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendeleza miradi ya umeme vijijini kwani si tu upatikajaji wa nishati hiyo utanufaisha mtu mmoja mmoja, bali pia hata utendaji wa taasisi mbalimbali nao utaimarika

**TZ&BEYOND:** Kwa maelezo hayo Dkt. Ni wazi muda uliosalia wa utawala wa Rais Samia, unaweza kuwa na matokeo makubwa kwa Taifa?

**DKT. MATIKO:** Naliona hilo kwa sasa, sijui huenda akaja kubadilika, lakini nikiuangalia mwendo wake namwona kama kiongozi mwenye dhamira ya dhati ya kumkomboa Mtanzania na uzuri wenzetu wa Zanzibar si wanafiki, hawapendi kona kona, kama hawezi atasema siwezi na kama hataki wala hatakuzungusha. Naiona nchi ikipiga hatua kubwa baada ya muda wake wa sasa na hata huku baadae kama Mungu atamjaalia uzima na kuchaguliwa kuongoza nchi kwa kipindi cha pili.



**Rais Samia akiwa na Kiongozi Mkuu Oman Sultan Haitham bin Tariq Al Said mara baada kuwasili Al Alam Muscat**



**Rais Samia Hassan akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyeji wake Kiongozi Mkuu wa Taifa la Omani Sultan Oman Haitham bin Tariq Al Said kabla ya kuanza mazungumzo**



**Rais Samia akiwa amesimama pamoja na Mwenyeji wake Kiongozi Mkuu wa Taifa la Omani Sultan Haitham bin Tariq Al Said wakati Wimbo wa Taifa wa Tanzania**

# SIKU 365 ZA MAFANIKO 10 YA NGUVU

Mambo mengi yametekelezwa katika siku 365 za uongozi wa serikali ya awamu ya sita.
Uwapo wa Rais Samia madarakani, umeifanya nchi kuandika historia mpya ya mabadiliko ya uongozi bila kwenda kwenye sanduku la kura, ambapo aliyekuwa Makamu wa Rais aliapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Historia hiyo mpya ya Tanzania ilianza kwa Makamu wa Rais kukabidhiwa nchi kwa nafasi ya Kaimu Rais kwa muda wa siku mbili, Machi 17 na 18, 2021.

Machi 19,2021, alikula kiapo cha Rais ikiwa ni uhalalisho wa kushika rasmi madaraka ya juu kabisa kushikwa na kiongozi mwanamke katika ukanda wa Afrika Mashariki na katika nchi zinazounda Jumuiya ya Ushirikiano wa Maendeleo wa nchi za Kusini mwa Afrika, SADC.

Rais Samia alimteua Dkt. Philip Isidor Mpango ambaye alikuwa waziri wa Fedha na Mipango katika serikali ya awamu ya Tano kuwa Makamu wa Rais akichukua nafasi aliyoiacha yeye mwenyewe baada ya kuapishwa na kuwa Rais.

Katika hali isiyotarajiwa baada ya kushika dola alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri alilohudumu sanjari na mtangulizi wake.

Uamuzi wake huo ulibeba sura ya ukomavu wa kisiasa kwani timu hiyo ilitokana na uteuzi wa Hayati Rais Magufuli.

Na kwa sababu hizo alionesha dhamira ya kuendelea na Waziri Mkuu aliyetokea awamu ya tano na baadhi ya mawaziri na manaibu mawaziri, ingawa alifanya mabadiliko madogo kutokana na kuwapo kwa nafasi ya wazi ya waziri wa Fedha baada ya aliyekuwepo kumteuwa kuwa Makamu wa Rais.

Kipindi cha mabadiliko ya uongozi kilitokea muda mfupi kabla nchi haijaenda kwenye mchakato wa Bajeti na Mipango na huo ulikuwa mtihani wa kwanza kwa serikali ya Awamu ya Sita pamoja na vita dhidi ya Covid 19.

Haikuchukua muda serikali iliwezesha upatikanaji wa Bajeti na Mpango kupitia Bunge la Tanzania, na hatimae dira na mwelekeo wa serikali ya Awamu ya Sita ulihabarishwa kwa hotuba iliyotolewa bungeni na Rais Samia.

Hotuba hiyo ilisheheni vipaumbele na mwelekeo mpya wa kujenga uchumi na ustawi wa watu, hali kadhalika mapambano dhidi ya Corona.



# MIRADI 10 YA KIMKAKATI




UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA MSALATO







UPANUZI WA LANGO LA BAHARI YA DAR ES SALAAM



UJENZI WA BARABARA KUU DODOMA



UJENZI WA NJIA ZA MABASI YAENDAYO HARAKA





UJENZI WA KIWANDA KIKUBWA CHA MBOLEA MTWARA



MRADI WA BANDARI YA BAGAMOYO (MCHAKATO UNAENDELEA)





UJENZI WA RELI YA KISASA -SGR





UJENZI WA BWAWA LA KUFUA UMEME LA NYERERE-RUFIJI





MRADI WA GESI ASILIA KITUO CHA MKUCHINGA NA LIKONGO



MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI KUTOKA UGANDA HADI TANZANIA

KUTOKA KWA

# Mhariri Mtendaji

## SGR NI CHACHU YA MAENDELEO

MRADI wa ujenzi wa reli ya kisasa maarufu kama SGR unakwenda kwa kasi na hakuna ubishi wowote mradi huo utakamilika kwa wakati na muda sahihi.

Mamilioni ya watanzania matumaini na hamu yao ni kuona mradi huo unaanza kufanya kazi ili iwawie rahisi kuutumia katika usafiri na usafirishaji.

Hakuna hata mtanzania mmoja asiyetaka kufaidi matunda ya SGR ambayo tumeambiwa ina uwezo wa kuhimili kubeba magari moshi yenye mabehewa mengi ya abiria na mizigo kwa wakati mmoja.

Sisi Jarida la TZ&BEYOND tunaamini ujenzi wa mradi huu ambao ni wa kimkakati unayo tija kubwa kwa nchi na wananchi.

Ikumbukwe kuwa kwa sasa dunia imeshahamia kwenye usafiri wa reli za kisasa, hii inamaanisha hata sisi hatupaswi kujichelewesha.

Kasi ya ujenzi wa mradi huu hapa Tanzania unatusukuma kutoa pongezi za dhati kwa serikali ya Awamu ya Tano iliyokuwa chini ya Hayati Rais Dkt. John Magufuli na pia kwa serikali ya Awamu ya Sita ambayo iko chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwenda na kasi ya maendeleo ya dunia.

Kukamilika kwa ujenzi huo wa reli ya kisasa (SGR) nchini hakutainufaisha Tanzania pekee, bali hata nchi jirani zitanufaika na ujenzi wake.

Reli hii yenye upana wa mita 1.435, inatarajiwa kubeba mamilioni ya abiria na mizigo zaidi ya tani milioni 17 kwa mwaka.

Jarida la TZ&BEYOND tunaamini mradi huu mkubwa na wa muhimu utakuwa chachu na kichocheo cha maendeleo kwa watanzania wote, hivyo basi ni jukumu letu kuunga mkono, kuulinda na kuuthamini ili utuletee tija kusudiwa.

Aidha tunaiona haja ya kumpongeza Rais Samia kwa utayari wake wa kuuendeleza mradi hu una miradi mingine yote ya kimkakati.

**Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.**





**Jimmy C. Kiango**
**MHARIRI MTENDAJI**

TRA
TANZANIA REVENUE AUTHORITY
ISO 9001: 2008 Certified

VISION PLUS
EYE CLINIC

KCB BANK

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

CRDB BANK
Tunakusikiliza

BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

# SHUKRANI

za dhati kwa WASHIRIKA WETU




# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK
The bank that listens